

Vituo vya Nishati vya Jamii vimeanzishwa ili kutoa huduma kwa jamii za vijijini Oldonyosambu na Ngarenanyuki.

Tekinolojia mbali mbali huonyeshwa au kuuza kwenye vituo hivyo. Tekinolojia hizo ni pamoja na

- Aina za majiko yanayopunguza moshi ndani ya nyumba na kutumia kiasi kidogo cha kuni
- Chombo kidogo cha umemejua kwa ajili ya mwanga, kuchaji betri na simu
- Mtambo wa gesi ya kinyesi kwa kupikia
- Mazao yaliyohifadhiwa au kusindikwa na vikundi vya ushirika wa akina mama vijijini: sabuni za mbono na mboga zilizohifadhiwa kwa matumizi ya muda mrefu
- Maelezo kuhusu nishati mbadala, mtandao wa kimataifa wa kompyuta (intaneti)
- Maktaba ndogo ya nishati na mazingira



The European Union's 9th EDF Energy Facility Programme

## Punguza moshi refusha maisha:

Kampeni ya kupunguza moshi ndani ya nyumba na kuhamasisha jamii za vijijini Tanzania kutumia nishati mbadala.

Mradi wa Nishati Mbadala (BEST RAY) umefadhiliwa na Tume ya Jumuiya ya Ulaya

## Tembelea VITUO VYA NISHATI VYA JAMII VILIVYOPO

- Oldonyosambu sokoni
- Ngarenanyuki jirani na Ofisi ya Kata



This project is funded by  
The European Union



# Punguza moshi Refusha maisha

**Mradi wa Nishati Mbadala  
A best ray project activity**



*Mama yangu ana 'jiko janja'*

# Kwaheri mafiga matatu

Epuka athari za moshi ndani ya nyumba.


Moshi husababisha kupoteza maisha katika jamii.

Moshi huleta athari za kiafya zifuatazo: magonjwa ya kupumua, kukohoa, saratani, magonjwa ya mapafu, pumu, nimonia, vichomi na matatizo ya macho.

Magonjwa ya kupumua huuwa watu wengi vijijini.

Magonjwa mengine yanayosababishwa na moshi kama saratani na magonjwa ya kupumua hayana dawa.

**Muone daktari ukipata maumivu.**



# Jiko janja ni rafiki yako.



... lakini naupenda moshi kwa sababu...



**Unafukuza wadudu.** Weka wanyama nje kwenye mabanda yao ili kupunguza idadi ya wadudu ndani ya nyumba. Tumia mimea ya asili kufukuza wadudu. Tembelea Kituo cha Nishati cha Jamii kujifunza matumizi ya mimea mbali mbali.

**Ninatumia majivu kuyafanya maji kuwa ya rangi.** Mchaichai ni chaguo zuri zaidi. Unaoengeza afya na hufukuza wadudu. Jipatie mche wa mchaichai wakati wa kampeni ya Mradi au tembelea Kituo cha Nishati cha Jamii.

**Ninatumia majivu kuponyesha maumivu ya tumbo.** Tumia mimea kama Alovera kuponyesha maumivu. Moshi siyo dawa. Moshi huathiri afya yako.

**Ninatumia moshi kuhifadhi mazao.** Tumia kaushio la jua au jenga chumba cha kukaushia nje ya nyumba. Utakuwa na afya na utahifadhi mazao kwa ufanisi zaidi.

Jenga jiko janja nyumbani kwako.

Jiko janja hujengwa kwa matofali ya kuchoma au kwa udongo na hutoa moshi nje. Kwa nyongeza, jiko janja huhifadhi joto ndani ya nyumba kwa muda mrefu, linatumia kiasi kidogo cha kuni kwa kupikia, na hupika kwa muda mfupi.

Mradi wa Nishati Mbadala unatoa fursa ya kupata jiko janja kwa matumizi ya nyumbani. Mradi unalipia gharama za ujenzi wa jiko hilo. Anayehitaji jiko janja atalipa 15000TSh tu kama mchango kwa ushirika wa akina mama watakaojenga jiko hilo.

Mpe afisa jamii wa mradi au mhudumu wa kituo cha nishati jina lako na namna ya mawasiliano. Utajengewa jiko ukiomba. Majiko yatajengwa kwa mchango wa Mradi kwa watu 200 tu watakao omba kwanza.